TANGAZO LA SERIKALI NA. 651 la tarehe 18/11/2022

SHERIA YA BARABARA,
(SURA YA 167)

# NOTISI

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 11*)

NOTISI YA KUPANGA BARABARA KATIKA MADARAJA STAHIKI YA MWAKA 2022

Jina

1. Notisi hii itaitwa Notisi ya Kupanga Barabara katika Madaraja Stahiki ya Mwaka 2022.

Kupanga barabara kwenye madaraja stahiki

2.-(1) Barabara zilizotajwa katika Jedwali la Kwanza la Notisi hii zinaainishwa kuwa barabara za mkoa.

(2) Barabara zilizotajwa katika Jedwali la Kwanza la Notisi hii zilikuwa chini ya mamlaka ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini zinawekwa kuwa chini ya Wakala wa Barabara wa Tanzania.

**JEDWALI LA KWANZA**

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 2(1)*)

**Barabara Zilizopangwa Katika Daraja la Barabara za Mikoa**

| NA. | JINA LA BARABARA | UREFU (KM) | MKOA |
|---|---|---|---|
| 1. | Tanzanite road(Ally Hassan Mwinyi Road Junction-Tanzanite Bridge-Toure Road Junction-Haile Selassie Road-Yatch Club Road-Kimweri-Jitegemee Road-Shama Road (TANESCO - Old Bagamoyo Road Junction) | 13.07 | DAR ES SALAAM |
| 2. | Baraza la Maaskofu - Nyerere Bridge (Kigamboni) | 5.23 | DAR ES SALAAM |

*Tangazo la Serikali na. 651 (linaendelea)*

**JEDWALI LA PILI**

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 2(2)*)

**Barabara zilizopangwa chini ya Mamlaka ya Wakala wa Barabara Tanzania.**

| NA. | JINA LA BARABARA | UREFU (KM) | MKOA |
|---|---|---|---|
| 1. | Kakozi-Ilonga | 50.1 | SONGWE |
| 2. | Maandazi-Kimweri-CCBRT-Haile Selassie-Ghuba | 2.3 | DAR ES SALAAM |
| 3. | Sima-Tunyenye-Isole | 29.5 | MWANZA |

Dodoma,
4th October, 2022

MAKAME M. MBARAWA
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*